

336/1
KISWAHILI
Karatasi ya Kwanza
2024
Saa 2



UGANDA NATIONAL EXAMINATIONS BOARD
Uganda Certificate of Education

KISWAHILI

Karatasi ya Kwanza
Insha na Ufupisho

Saa mbili

MAAGIZO KWA WATAHINIWA:

Karatasi hii ina sehemu; mbili: A na B.

Jibu maswali mawili kwa ujumla.

Katika sehemu A, kuna maswali mawili. Chagua swalii moja.

Sehemu B ni ya lazima.

Majibu yote yaandikwe kwenye karatasi uliyopewa.

Swali la ziada halitasahihishwa.

SEHEMU A

UTUNZI WA INSHA

Ama

1. Watu wengi nchini hutumia vibaya mazingira wanamoishi. Tatizo hili limesababisha madhara mengi nchini. Kuna haja ya kuyaokoa mazingira. Andika insha ukipendekeza namna mazingira yanavyoweza kutunzwa.

Au

2. Jamii iko katika hatari kubwa ya kuathirika kutokana na ongezeko la matumizi ya madawa ya kulevya. Madawa hayo yanauzwa madukani na hata mitaani. Wewe kama kiongozi wa wanafunzi, andika ushauri mwafaka utakaowatolea wanafunzi wenzako kuhusu matumizi ya madawa ya kulevya.

SEHEMU B

UFUPISHO

3. *Kwa kutumia maneno sabini (70), eleza jinsi mtu anavyoweza kujilinda dhidi ya ugonjwa wa malaria kama ilivyoelezwa katika taarifa.*

Ugonjwa wa *malaria* ni hatari sana kwa mwanadamu. Ugonjwa huu umekuwa tishio kubwa kwa wana Uganda na ulimwengu mzima. Watu wengi, yaani watoto kwa wazee wamekufa kwa ugonjwa wa malaria.

Ugonjwa huu huambukizwa na mbu wa kike anayejulikana kama anofelesi. Mbu hupenda kuishi kwenye mahali yenye majimaji na vichaka. Mahali hapo panakuwa kama maskani yao ambapo wanataga mayai na kuzalia hapo.

Baadaye, mbu hawa hukua na kuanza kwenda penye giza wakati wa usiku kama kwenye nyumba na kwenye miti. Binadamu asipolala ndani ya chandarua anaumwa na mbu wakati wa usiku akiwa amelala.

Mbu yule wa aina ya anofelesi akikuuma ataingiza virusi nya malaria mwilini mwako na utapata ugonjwa huo wa malaria. Aidha, kutofunga milango na madirisha jioni husababisha mbu kuingia kwa nyumba na kujificha humo.

Kutokana na madhara yanayosababishwa na mbu hao hatari, ni muhimu kujikinga dhidi ya wadudu hao kwa kutunza usafi nyumbani ili tuweze kujilinda dhidi ya ugonjwa wa malaria.

Njia ya kwanza, inatubidi kufyeka nyasi zilizo karibu na nyumba zetu ili tusiwape mbu nafasi ya kujificha na kuzaana. Kwa kufanya hivyo, tutawazuia mbu kujificha humo. Isitoshe, ni muhimu kutoa maji yaliyotuama

karibu na nyumba zetu. Tunaweza kufanya hivi kwa kutoa vyombo visiviyotumika kama chupa, ndoo na beseni ili mbu wasizalie humo mayai yao.

Ni jambo la muhimu kufunga milango na madirisha wakati wa jioni ili mbu wasiingie kwa nyumba. Pamoja na hayo, tunasitahili kulala ndani ya vyandarua ili tusiumwe na mbu hao hatari.

Njia nyingine ya kujikinga dhidi ya wadudu hao hatari, tunaweza kunyunyiza dawa nyumbani na kuwaua. Pia, ni vizuri kufunika mashimo yaliyo karibu na nyumbani kwetu ili mbu wasije wakazalia humo.

Mtu aliye na ugonjwa wa malaria anaonesha dalili zifuatazo; kwanza mtu huyo atakuwa na udhaifu wa mwili, kuhisi baridi kila wakati, maumivu ya kichwa, joto kali mwilini na kutokuwa na hamu ya kula.

Ni muhimu kwamba ukijitambua kuwa na dalili yoyote ya ugonjwa wa malaria uende hospitalini upimwe na kupata matibabu.

Mwishoni, wizara ya afya inastahili kuelimisha watu kujikinga dhidi ya ugonjwa wa malaria na magonjwa mengine kwa kutumia vyombo vyaa mawasiliano kama magazeti, radio na televisheni.